**TANGAZO LA SERIKALI NA. …. la tarehe …………**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),**

**SURA 288**

**KANUNI**

**Zimetungwa chini ya Kifungu ……**

# KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA MWENYEKITI WA KITONGOJI KATIKA MAMLAKA ZA MIJI ZA MWAKA, 2009

Jina

1. Kanuni hizi ziitwe Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka, 2009.

Tarehe ya kuanza kutumika

2 Kanuni hizi zitatumika katika Vijiji na Vitongoji vyote vilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Miji na zitaanza kutumika tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3 Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyotamkwa vinginevyo;

"Afisa Mtendaji wa Kata" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kata na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata kwa mujibu wa Kanuni hizi;

Sura 258

"Afisa Mtendaji wa Kijiji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kijiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji kwa mujibu wa Kanuni hizi;

Sura 288

"Chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

RASIMU

Sura 288

"Kijiji" maana yake ni kijiji kilichomo katika eneo la Mamlaka za Miji ambacho kinatambuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Kitongoji" maana yake ni sehemu ya Kijiji kinachotambuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)

"Mahali pa matangazo ya uchaguzi" maana yake ni sehemu iliyotengwa maalum au iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo, taarifa za Kijiji au Kitongoji na taarifa mbalimbali za uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Kijiji au Kitongoji na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Kijiji au Kitongoji;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi" maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kijiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi wakati wa uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

Sura 357

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji ambamo kuna vijiji au vitongoji vinavyofanya uchaguzi na ni pamoja na Afisa mwingine wa Umma aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Raia" maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

"Orodha ya wapiga kura" maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

" Siku ya uteuzi" maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea;

"Uchaguzi" maana yake ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji;

"Wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao uchaguzi wa kawaida au uchaguzi mdogo unatakiwa ufanyike kwa mujibu wa

RASIMU

Kanuni hizi na unaanzia tarehe ambayo Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya uchaguzi na kumalizika mara baada ya kutangaza majina ya wagombea waliochaguliwa."

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Kuzingatia Sheria, Kanuni, matangazo na maelekezo

4. Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa na Afisa mwingine wa umma atakayehusika na uendeshaji wa uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia uchaguzi huo kwa kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Tangazo la uchaguzi kwa umma

5. (1) Waziri atatoa Tangazo la Uchaguzi kwa umma katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa Nchi nzima siku tisini (90) kabla ya siku ya Uchaguzi ili umma uweze kujiandaa kwa ajili ya Uchaguzi.

(2) Tangazo litakalotolewa na Waziri kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii litaelekeza mambo yafuatayo:-

a. ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika; na

o masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji

6. (1)Utafanyika Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji katika kila Kijiji na kila Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza majina na mipaka ya Vijiji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika katika mahali pa matangazo ya Uchaguzi siku hamsini (50) kabla ya kutoa maelekezo kuhusu Uchaguzi.

(2) Utafanyika Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji kwa kila Kitongoji na kila Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza majina ya mipaka ya Vitongoji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika katika mahali pa matangazo ya uchaguzi siku ishirini na moja (21) kabla ya kutoa maelekezo kuhusu Uchaguzi.

Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

7 (1) Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji hawatapungua 15 na hawatazidi 25, ambao ni:-

RASIMU

c. Mwenyekiti wa Kijiji;
d. Wenyeviti wa Vitongoji vilivyomo katika eneo la Kijiji; na
e. Wajumbe watakaochaguliwa wakiwemo wanawake ambao idadi yao haitakuwa chini ya robo ya wajumbe wote wa Halmashauri ya Kijiji.

(2) Afisa Mtendaji wa Kijiji atakuwa Katibu wa Halmashauri ya Kijiji.

Maelekezo kuhusu uchaguzi

8 (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya uchaguzi siku zisizopungua 28 kabla ya siku ya uchaguzi.

(2) Maelekezo ya uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hii yataelekeza mambo yafuatayo:

a. tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi;
b. muda na sehemu ya kuandikishia wapiga kura

c. muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;

d. kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura

washiriki uchaguzi;

e. kuwataka wakazi wenye umri wa miaka 21 au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji wachukue fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

f. tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kuagiza kwamba muda wa kuchukua na kurudisha

RASIMU

fomu za kugombea hautazidi siku saba (7);

g. siku ambayo uteuzi utafanyika na mahali pa matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa ili wapiga kura wazione;

h. muda wa kutoa pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;

i. tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

j. kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi ambacho hakitazidi siku saba (7) kuanzia tarehe ya uteuzi; na

k. masuala mengineyo yanayohusiana na Uchaguzi.

Orodha ya wapiga kura

9. 1. Uandikishaji wa Orodha ya wapiga kura katika Kitongoji kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji,Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji utafanyika siku sitini (60) kabla ya siku ya uchaguzi na utafanywa na watumishi wa umma.Watendaji wa vijiji, Mitaa na Kata hawataruhusiwa kuandikisha na kuandaa orodha ya wapiga kura

o Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajiri.

RASIMU

3. Vituo vya uandikishaji wa orodha ya wapiga kura vitafunguliwa kuanzia saa 1.30 asubuhi na kufungwa saa 12.00 jioni.

4. Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa vyama vya Siasa.

5. Vituo vya uandikishaji wa orodha ya Wapiga Kura vitafunguliwa kuanzia saa 1.30 asubuhi na kufungwa saa kumi(10:00) jioni

6. Vyama vya siasa vitaruhusiwa kuwepo wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

7. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika mahali pa matangazo ya uchaguzi orodha ya wapiga kura na kutunza kumbukumbu yake.

8. Mkazi yeyote wa Kitongoji au vyama vya siasa vitakuwa na haki ya kukagua orodha na Orodha ya wapiga kura katika muda wa siku nne (4) tangu tarehe orodha ya wapiga kura ilipobandikwa mahali pa matangazo ya uchaguzi ili kutoa pingamizi au maoni ya usahihi wa Orodha hiyo na anaweza kuomba:-

(a) Orodha irekebishwe kwa kuongeza jina lake au jina la mkazi; na

(b) Orodha irekebishwe kwa kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa hana sifa

RASIMU

ya kupiga kura katika Kitongoji husika.

(5) Pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atalitolea uamuzi na kurekebisha orodha ya wapiga kura iliyotangazwa katika muda wa siku tano (5) kuanzia tarehe ya kuwasilishwa pingamizi hilo.

(6) Mtu yeyote au chama cha siasa ambacho hakitaridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kitawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ataishughulikia rufaa hiyo katika muda wa siku tano (5) baada ya kupokea rufaa hiyo.

(7) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (6) ya kanuni hii utakuwa wa mwisho.

Sifa za wapiga kura

10. Mkazi yeyote wa Kitongoji atakuwa na haki ya kupiga kura ikiwa:-

. ni raia wa Tanzania;
a. ana umri wa miaka 18 au zaidi;
b. ni mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji; na
c. hana ugonjwa wa akili.

Kupoteza sifa

11. Mkazi yeyote wa Kitongoji hatakuwa na haki ya kupiga kura ikiwa:-

d. si raia wa Tanzania;
e. hajatimiza umri wa miaka 18;
f. si mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji; na
g. ana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Sifa za mgombea

12 (1) Mkazi yeyote wa Kitongoji anaweza kugombea uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji ikiwa:-

h. ni raia wa Tanzania;
i. ana umri wa miaka 21 au zaidi;
j. ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
k. ana kipato halali cha kumwezesha kuishi;
l. ni mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji;
m. ni mwanachama na amedhaminiwa na chama cha siasa;

RASIMU

n. asiwe amepatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu na kuhukumiwa adhabu ya kifungo cha miezi 6 au zaidi au adhabu ya kifo; na

o. hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Siku ya uteuzi

13. (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji siku zisizopungua ishirini (20) kabla ya tarehe ya Uchaguzi.

2. Siku ya uteuzi, wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya saa kumi (10.00) kamili jioni baada ya hapo fomu hazitapokelewa ili kuruhusu kufanyika kwa uteuzi wa wagombea kutokana na fomu zilizowasilishwa.

3. Saa ya uteuzi itakuwa kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi hadi saa kumi na dakika kumi na tano (10.15) jioni ya siku ya uteuzi.

4. Baada ya uteuzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika mahali pa matangazo ya uchaguzi majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji.

5. Ikiwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, utaratibu wote wa uteuzi utaanza upya.

Kutengua uteuzi

14. (1) Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kijiji kutokana na kifo au sababu nyingine yeyote, Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kufanya uteuzi mpya siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu siku ya uteuzi uliotenguliwa.

(2) Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kitongoji kutokana na kifo au sababu nyingine yeyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kufanya uteuzi mpya siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu siku ya uteuzi uliotenguliwa

(3) Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na wagombea wa ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kutokana na kifo au sababu nyingine yoyote Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo

RASMI

zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(4) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kijiji kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(5) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kitongoji kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

6. Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

Pingamizi dhidi ya uteuzi

15. (1) Mgombea ambaye hakuteuliwa na ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kujaza fomu ya pingamizi na kumtaka Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamteua au atatengua uteuzi uliofanyika kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni hizi.

2. Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii itawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili (2) tangu uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili (2) kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

3. Mgombea au mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 16 katika muda usiozidi siku nne (4) kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

4. Kamati ya Rufaa itasikiliza na kutoa uamuzi kuhusu

uteuzi wa mgombea katika muda usiozidi siku nne (4) tangu siku ya kupokea rufaa.

5. Uamuzi wa Kamati ya Rufaa kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la uteuzi utakuwa wa mwisho.

6. Mgombea au mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua kesi Mahakama ya Wilaya baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

Kamati ya Rufaa

16 7. Kutakuwepo na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya itakayoteuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa ambayo itasikiliza malalamiko ya uteuzi wa mgombea wa uchaguzi katika kila Wilaya.

2. Kamati ya Rufaa itateuliwa siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.

3. Kamati ya Rufaa itakayoteuliwa kwa mujibu wa kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa na wajumbe wafuatao:-

. Katibu Tawala wa Wilaya au Afisa mwingine wa umma atakayeteuliwa ambaye atakuwa mwenyekiti;

a. Viongozi wawili (2) wa dini kutoka madhehebu tofauti yaliyopo katika eneo la wilaya;

b. Afisa yeyote kutoka taasisi ya umma iliyoko katika wilaya husika; na

c. Afisa yeyote wa umma anayefanya kazi katika ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa katibu isipokuwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

4. Bila kuathiri kanuni ndogo ya 3 ya kanuni hizi, endapo mojawapo ya nafasi ya wajumbe waliotajwa kwenye kanuni ndogo ya 3 ya kanuni hizi haipo katika eneo la wilaya basi uteuzi wa mjumbe utazingatia hali halisi ya eneo husika.

RASIMU

**Utashi wa wajumbe wa Kamati ya Rufaa**

17. Mtu yeyote hatateuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Rufaa iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 16 endapo:-

(a) anahusika na uteuzi wa wagombea;

(b) ni Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(c) ni kiongozi wa ngazi yeyote wa chama cha siasa; na

(d) ni mtumishi wa Halmashauri.

**Kampeni za uchaguzi**

18. (1 ) Kampeni za uchaguzi zitaanza siku moja (1) baada ya uteuzi wa wagombea na zitamalizika siku moja (1) kabla ya siku ya uchaguzi.

(2) Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa kufuata ratiba itakayowasilishwa na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa na kuratibiwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha ratiba ya kampeni za uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye atahakikisha kunakuwepo ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni.

(4) Ratiba ya kampeni za uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi itakuwa taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi.

(5) Kampeni za uchaguzi zitaanza saa mbili (2.00) asubuhi mpaka saa kumi na moja (11.00) jioni ya kila siku ya kampeni.

**Masharti ya kampeni**

19 Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa kutumia rushwa, takrima, kashfa, lugha za matusi, ubaguzi wa kijinsia, kidini, ukabila au wa namna yoyote ile ambao matokeo yake ni kumbagua mtu.

**Utaratibu wa kupiga kura**

20 0. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa viti maalum wanawake, utafanyika katika vitongoji vilivyomo katika Kijiji.

RASIMU

2. Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna ya kumwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa.

3. Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililowazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

4. Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajampatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, atajiridhisha kama jina la mpiga kura limeorodheshwa katika orodha ya wapiga kura

5. Bila kuathiri Kanuni Ndogo ya (4) hapo juu, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza pia kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye orodha ya wapiga kura.

6. Aina ya vitambulisho ambavyo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe ni pamoja na vifuatavyo:

. kitambulisho cha mpiga kura;
a. kitambulisho cha kazi;
b. hati ya kusafiria;
c. kadi ya benki;
d. kadi ya bima ya afya; au
e. kitambulisho cha shule au chuo.
f. Leseni ya udereva.

RASIMU

7. Ikiwa mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote, lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, utambuzi utafanywa na wakazi wa eneo husika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamruhusu mtu huyo kupiga kura.

8. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atampatia mpiga kura karatasi nne (4) za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo:-

. Mwenyekiti wa Kijiji;
a. Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;
b. Wajumbe wa viti maalum wanawake; na
c. Mwenyekiti wa Kitongoji.

9. Kura zitapigwa kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi mpaka saa nane (8.00) mchana.

10. Kura zitakuwa za siri na zitapigwa katika majengo ya umma au sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataiteua baada ya kushauriana na wagombea au wawakilishi wao au vyama vya siasa.

11. Siku ya kupiga kura, endapo atatokea mpiga kura ambaye ana ulemavu wa macho au ulemavu wowote wa kimaumbile au hajui kusoma na kuandika, anaweza kumuomba mtu aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, mgombea au mwakilishi wake.

Karatasi za kura

21 12. Kutakuwa na karatasi za kawaida za kupigia kura ambazo zitakuwa na nembo ya Halmashauri husika kama zinavyooneshwa kwenye fomu chini ya Kanuni hizi.

2. Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii karatasi za kupigia kura zitakuwa na sifa



RASIMU

zifuatazo:

i. Sehemu mpiga kura atakapoandika jina la mgombea anayempigia kura;

b. Sehemu ambapo mpiga kura ataandika jina la chama cha siasa cha mgombea aliyempigia kura; na

c. uwezo wa kukunjwa kwa urahisi.

Kuhesabu kura 22 9. Wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kuwepo katika kituo cha kuhesabia kura:-

. Msimamizi wa Uchaguzi;

b. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

c. mgombea;

d. mwakilishi wa mgombea;

e. Polisi, Mgambo au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na

f. Mwangalizi wa Uchaguzi.

2. Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajaanza kuhesabu kura, atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au wawakilishi wao:-

. kuhakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

b. atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;

c. atakagua lakiri na kuona kama imefunguliwa au haijafunguliwa;

d. atakata lakiri; na

e. atafungua sanduku la kupigia kura.

3. Kura zitahesabiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwenye Kitongoji ambako Uchaguzi umefanyika mbele ya wagombea au wawakilishi wao.

RASIMU

**Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji**

23 4. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

2. Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi ambaye atatangazwa kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

3. Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji yatajazwa kwenye fomu maalum ambayo itasainiwa na wagombea au wawakilishi wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo.

**Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji**

24 (1) Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa Viti Maalum Wanawake yatajazwa kwenye fomu maalum ambayo itasainiwa na wagombea au wawakilishi wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo na nakala kuwasilishwa ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa ajili ya kujumlishwa na kutangaza mshindi au washindi wa kila nafasi iliyogombewa

(2) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume utakuwa kama ifuatavyo:

. endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;

b. endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

RASIMU

c. endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji; na

d. endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza mshindi na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao, ambao watatangazwa kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

(3) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi la wagombea wa viti maalum wanawake utakuwa kama ifuatavyo:-

. endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;

b. endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

c. endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi wa Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji; na

d. endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wote au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza

matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao ambao watatangazwa kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

**Utaratibu wa kutangaza matokeo ya mwenyekiti**

25 1. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na kujaza jumla ya kura katika fomu maalum.

o Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji.

3. Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi ambaye atatangazwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji.

**Matendo yasiyobatilisha matokeo ya uchaguzi**

26 Kwa mujibu wa Kanuni hizi, kutokuwepo kwa wagombea au wawakilishi wao wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo au kukataa kusaini fomu ya matokeo hakutazuia wala kubatilisha utekelezaji wa shughuli yoyote ya uchaguzi.

**Kuahirisha upigaji kura**

27. Siku ya kupiga kura endapo litatokea tukio litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ili mradi zisizidi siku saba (7) tangu siku ya uchaguzi ulipoahirishwa.

**Malalamiko kuhusu uendeshaji wa uchaguzi**

28. (1) Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uendeshaji wa uchaguzi atakuwa na haki ya kupeleka malalamiko yake Mahakama ya Wilaya katika muda wa siku thelathini (30) baada ya siku ya kutangaza matokeo ya uchaguzi.

2. Malalamiko ya uchaguzi yatakayowasilishwa Mahakama ya Wilaya ni yale tu yatakayokuwa yanahusu ukiukwaji wa utaratibu wa uchaguzi uliowekwa na Kanuni hizi.

**Nafasi wazi**

29. (1) Nafasi ya uenyekiti na ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au ya uenyekiti wa Kitongoji itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:-

RASIMU

b. kifo cha mwenyekiti au mjumbe;

c. mwenyekiti au mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;

d. mwenyekiti au mjumbe kuondokewa na sifa za kuwa mgombea;

e. kubatilishwa kwa matokeo ya uchaguzi;

f. kukoma kuwa mwanachama wa chama cha siasa

kilicho mdhamini;

f. kuhama Kijiji au Kitongoji;

g. endapo Mwenyekiti hataitisha mikutano mitatu (3) ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi; na

h. endapo mwenyekiti au mjumbe hatahudhuria mikutano mitatu (3) ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu ya msingi.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii, Afisa Mtendaji wa Kijiji atatoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri katika kipindi kisichozidi siku saba (7) tangu kutokea kwa jambo hilo.

Uchaguzi mdogo

30. 1. Mkurugenzi wa Halmashauri atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji siku saba (7) baada ya kupokea taarifa toka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji juu ya kuwepo kwa nafasi iliyoachwa wazi.

o Nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa kwa kufanya uchaguzi mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.

3. Nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa katika muda wa siku sitini (60) baada ya kutangazwa kuwa wazi.

RASIMU

4. Hakuna nafasi ya uenyekiti au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itakayojazwa endapo muda uliobaki ni miezi sita (6) au pungufu yake kufikia siku ya kufanyika kwa uchaguzi wa kawaida.

| | | |
|---|---|---|
| Kiapo | 31 | Wafuatao watatakiwa kula kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Wakili, Wakili wa Serikali Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-<br>f. Msimamizi wa Uchaguzi;<br>g. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;<br>h. Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Rufaa; na<br>i. Afisa mwingine yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi. |
| Masharti ya kuwalinda wasimamizi wa uchaguzi na wajumbe wa Kamati ya Rufaa | 32 | (1) Hatua yoyote ya nidhamu au kiutawala itakayochukuliwa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au Afisa yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa uchaguzi ambayo itathibitika kwamba ni hatua za kulipa kisasi au kumkomoa mhusika itakuwa ni batili na yeyote atakayehusika kuchukua hatua hizo atakuwa ametenda kosa la jinai chini ya Kanuni hizi.<br>(2) Mtu au taasisi yoyote itakayokiuka Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii ikipatikana na hatia itahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi Shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote yaani faini na kifungo. |
| Watazamaji wa ndani na nje wa uchaguzi | 33 | 0. Watazamaji wa ndani na wa nje watakaopenda kutazama uchaguzi wataruhusiwa kufanya hivyo baada ya kupata kibali cha Msimamizi wa Uchaguzi.<br>2. Watazamaji wa uchaguzi wa ndani na nje watafanya shughuli zao za utazamaji kwa gharama zao wenyewe. |

RASIMU

Makosa ya uchaguzi

34 (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda makosa ya uchaguzi ikiwa:-

f. ataharibu orodha ya wapiga kura;
g. atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea uenyekiti au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Mwenyekiti wa Kitongoji;
h. ataharibu karatasi za wagombea;
i. ataghushi karatasi za uteuzi;
j. atapiga kura zaidi ya moja kwa ajili ya kumchagua mgombea mmoja;

f. atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga uchaguzi;

g. atafanya kampeni siku ya uchaguzi;

h. ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au chama cha siasa katika mita mia tatu (300) kutoka kwenye Kituo cha Uchaguzi;

i. atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi kutekeleza majukumu yake;
j. atakiuka masharti ya kiapo chake;
k. atafanya jambo lolote kinyume na Kanuni za Uchaguzi;

l. atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa mgombea mmoja; na

m. atavunja masharti ya kampeni za uchaguzi.

3. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Namba

35 Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka ya Miji za Mwaka 2004 zinafutwa.

318 na 319 ya

Mwaka

2004

**FOMU NA. 1**

## FOMU YA UCHAGUZI

## FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI/KIJIJI

***(Chini ya Kanuni ya 8(2) (d))***

Kitongoji……………………..

Kijiji…………………………

Kata………………………….

Mji/Manispaa/Jiji……..

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**

(Ijazwe na anayeomba kugombea)

1. Jina…………………………………………..
2. Jinsi (Me/Ke)...……………………………..
3. Uraia ………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa……...…………………...
5. Mahali unapoishi katika Kitongoji/Kijiji………………
6. Kazi/shughuli yako halali……………………
7. Uwezo wako wa kusoma na kuandika

   a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
   b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
   c. Kusoma Kiingereza Ndiyo/Hapana*
   d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

RASIMU

8. Jina la chama cha siasa…………………
9. Namba ya kadi ya uanachama………… tarehe ilipotolewa…………mahali ilipotolewa…………

10. Nathibitisha kwamba taarifa zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo Saini ……………………………tarehe ………

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

***(Chini ya kanuni ya8 (2) (d))***

(*Ijazwe na ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa …….ni mwanachama na amedhaminiwa na ………………………………

(*Taja jina la chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na chama cha siasa ………
3. Saini………………………….. Tarehe ………..
4. Wadhifa…………………………………………
5. Anwani:…………………………………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa………………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu………………………………………………………………
2. Muda (saa)………………………………………………………………………………..

RASIMU

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………………………………….
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………. ………………………
5. Tarehe……………………………………………………… ……………………
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au

mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji--------------------

**SEHEMU D: UTEUZI**

**(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)**

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa………………
2. Sababu……………………………………………

   ………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………
5. Tarehe……………..
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au

   mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………

RASIMU

**FOMU NA. II**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI/VITI MAALUM**

(*Chini ya Kanuni ya 8(2) d)*

Kijiji…………………………………………………...................
.

Kata……………………………………………..................

Mji/Manispaa/Jiji……………….............................
.

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**

(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina: ……………………………………………………………………………
2. Jinsi (Me/Ke)………………………………………………………………
3. Uraia …………………………………………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa …….……………………………………………………
5. Mahali unapoishi Kijiji……………………………………………………
6. Kazi/shughuli yako halali……………………………………………….
7. Uwezo wako wa kusoma na kuandika:

a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
c. Kusoma Kiingereza ndiyo/Hapana*
d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

8. Jina la chama cha siasa……………………

RASIMU

9. Namba ya kadi ya uanachama……………… tarehe iliyotolewa…………….mahali ilipotolewa………
10. Nathibitisha kwamba taarifa zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo

Saini ……………………..tarehe ………………

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa………………………………..…ni Mwanachama na

amedhaminiwa na
…………………………………………………………..….

(*Taja jina la chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na chama cha siasa ………
3. Saini:…………………………Tarehe……………
4. Wadhifa……………………………………………
5. Anwani……………………………………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa………………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

**(***Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi***)**

1. Tarehe ya kupokea fomu…………………………
2. Muda (saa) …………………………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………….
5. Tarehe…………………..
6. Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………….

**SEHEMU D: UTEUZI**

RASIMU

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa…………………
2. Sababu…………………………………………………… …………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi……………
4. Saini ya Msimamizi wa Uchaguzi ……………………
5. Tarehe…………………………………………….
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………..

RASIMU

**FOMU NA. III**

## FOMU YA UCHAGUZI

### FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI

*( Chini ya Kanuni ya 8 (2) d)*

Kitongoji…………………………

Kijiji………………………………

Kata………………………………

Halmashauri ya ………………….

### SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA

(Ijazwe na anayeomba kugombea)

1. Jina……………………………………………
2. Jinsi(Me/Ke)..…………………………………
3. Uraia ……………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa……..…………………………
5. Mahali unapoishi katika Kijiji……………………
6. Kazi/shughuli yako halali…………………………
7. Uwezo wako wa Kusoma na Kuandika
    a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
    b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
    c. Kusoma Kiingereza Ndiyo/Hapana*
    d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

8. Jina la chama cha siasa……………………
9. Namba ya kadi ya uanachama…………….
10. Tarehe ilipotolewa……………mahali ilipotolewa……………

Nathibitisha kwamba taarifa zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo

Saini ……………………..tarehe ……………………

RASIMU

(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa ………………………….ni mwanachama na amedhaminiwa na ………………………………………………………

(*Taja jina la chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na chama cha siasa ……………
3. Saini………………………….. Tarehe ………………
4. Wadhifa…………………………………………………
5. Anwani:…………………………………………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa………………

RASIMU

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu……………………………
2. Muda (saa)……………………………………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………
4. Saini ya Msimamizi wa Msaidizi Uchaguzi……………..
5. Tarehe…………………………………
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi au

   Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………………

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa……………………………………………
2. Sababu…………………………………………………………… …………..

……………………………………………………………………
……………..

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………....................................
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………………………
5. Tarehe……………………………………………………………………………..
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au

Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………………………….

RASIMU

**FOMU NA.IV**

**REJISTA YA WAPIGA KURA**

***( Chini ya kanuni ya 8 )***

Kitongoji/Kijiji…………………………………………..

Kata……………………………………………………

Mji/Manispaa/Jiji………………………………………
…

| Na. | Jina la Mpiga Kura | Jinsi | Umri | Nyumba/Kiwanja Na | Saini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

**FOMU NA V**

KARATASI ZA KUPIGIA KURA ZA MWENYEKITI WA KIJIJI

***(Chini ya Kanuni Na. 21)***

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA**

**MWENYEKITI WA KIJIJI OKTOBA, 2009**

| Nembo ya Halmashauri |
|---|

RASIMU

UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI

ANDIKA JINA LA MGOMBEA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MWENYEKITI WA KIJIJI

| 1 | **JINA LA MGOMBEA** | **JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA** |
|---|---|---|
| | | |

RASIMU

**FOMU NA VI**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MJUMBE WA HALMASHAURI**

Nembo ya Halmashauri

**ANDIKA JINA LA MGOMBEA UNAYEMPIGIA KURA KUWA MJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI.**

| | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |

RASIMU

**FOMU NA VII**

KARATASI ZA KUPIGIA KURA ZA MWENYEKITI WA KITONGOJI

***(Chini ya Kanuni Na. 21)***

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI OKTOBA, 2009**

| Nembo ya Halmashauri |
|---|

RASIMU

UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI

ANDIKA JINA LAMGOMBEA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MWENYEKITI WA KITONGOJI

| 1 | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA |
|---|---|---|
| | | |

**FOMU NA VIII**

KARATASI YA KUPIGIA KURA ZA WAGOMBEA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI VITI MAALUM

***(Chini ya Kanuni ya 21)***

Nembo ya Halmashauri

KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA

WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI VITI MAALUM OKTOBA, 2009

**ANDIKA JINA LA MGOMBEA UNAYEMPIGIA KURA KUWA MJUMBE VITI MAALUM KATIKA HALMASHAURI YA KIJIJI.**

| | **JINA LA MGOMBEA** | **JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA** |
|---|---|---|
| **1** | | |
| **2** | | |
| **3** | | |
| **4** | | |
| **5** | | |
| **6** | | |
| **7** | | |
| **8** | | |

RASIMU

**FOMU NAMBA IX**

FOMU YA MATOKEO YA MWENYEKITI WA KIJIJI/KITONGOJI

***(Chini ya Kanuni 23(1) na 25)***

| Na. | Jina la Mgombea | Chama cha Siasa | Kura alizopata | Saini ya Mgombea au Mwakilishi wake |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |

Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura………………………………………………..

Idadi ya waliopiga kura……………………………………………………………

Idadi ya kura zilizoharibika…………………………………………………………..

Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………………………....

Saini………………………………………………………tarehe…………………

Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi/Afisa Mtendaji wa Kijiji……………………………………………………………………………..

RASIMU

**FOMU NA. X**

FOMU YA MATOKEO YA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI/VITI MAALUM

***(Chini ya Kanuni 24(1))***

| Na. | Jina la Mgombea | Chama cha Siasa | Kura alizopata | Saini ya Mgombea au Mwakilishi wake |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |

Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura……………………………………..

Idadi ya waliopiga kura……………………………………………………

Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa………………………………………

Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………………….....

Saini……………………………………………………tarehe…………………

Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi/Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………………………………………………………..

RASIMU

**MIZENGO K. P.  PINDA (MB)**

**WAZIRI MKUU**

RASIMU

**DAR ES SALAAM**

**Tarehe……………….**

**TANGAZO LA SERIKALI NA. …. la tarehe ………….**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),**

---

**SURA 287**

---

**KANUNI**

---

**Zimetungwa chini ya Kifungu ……**

---

## KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA MWENYEKITI WA KITONGOJI KATIKA MAMLAKA ZA WILAYA ZA MWAKA, 2009

RASIMU

Jina

1. Kanuni hizi ziitwe Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka, 2009.

Tarehe ya kuanza kutumika

2 Kanuni hizi zitatumika katika Vijiji na Vitongoji vyote vilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Wilaya na zitaanza kutumika tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3 Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyotamkwa vinginevyo:-

"Afisa Mtendaji wa Kata" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kata na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Afisa Mtendaji wa Kijiji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kijiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji kwa mujibu wa Kanuni hizi;

Sura ya 258

"Chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Sura 287

“Kijiji” maana yake ni kijiji kilichomo katika eneo la Mamlaka za Wilaya na ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za

Sura 287 Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

“Kitongoji” maana yake ni sehemu ya Kijiji kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

“Mahali pa matangazo ya uchaguzi” maana yake ni sehemu iliyotengwa maalum au iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo, taarifa za Kijiji au Kitongoji na taarifa mbalimbali za uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

“Mkazi” maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Kijiji au Kitongoji na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au Taasisi iliyopo katika eneo la Kijiji au Kitongoji;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya na ni pamoja na afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi” maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kijiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi wakati wa uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

Sura 357 “Msimamizi wa Uchaguzi” maana yake ni Mkurugenzi, ambamo kuna vijiji vinavyofanya uchaguzi na ni pamoja na Afisa mwingine wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Raia” maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

“Orodha ya wapiga kura”maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa chini ya Kanuni hizi;

“ Siku ya uteuzi” maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea;

“Uchaguzi” maana yake ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na

RASIMU

Mwenyekiti wa Kitongoji;

"Wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao Uchaguzi wa kawaida au Uchaguzi mdogo unatakiwa ufanyike kwa mujibu wa Kanuni hizi na unaanzia tarehe Msimamizi wa Uchaguzi atakapotoa maelekezo ya uchaguzi na kumalizika mara baada ya kutangaza majina ya wagombea waliochaguliwa."

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana ya Serikali ya Mitaa.

Kuzingatia Sheria, Kanuni, matangazo na maelekezo

4. Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa na Afisa mwingine wa Umma atakayehusika na uendeshaji wa uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia uchaguzi huo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Maelekezo na Matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Tangazo la uchaguzi kwa umma

5. (1)Waziri atatoa Tangazo la Uchaguzi kwa Umma katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa Nchi nzima siku tisini (90) kabla ya siku ya Uchaguzi ili Umma uweze kujiandaa kwa ajili ya Uchaguzi.

(2) Tangazo litakalotolewa na Waziri kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya (1) ya Kanuni hii litaelekeza mambo yafuatayo:

a. ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika; na

b. masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji

6 2. Utafanyika Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji katika kila Kijiji na kila Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza majina na mipaka ya Vijiji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika katika mahali pa matangazo ya Uchaguzi siku hamsini (50) kabla ya siku ya Uchaguzi.

Wajumbe wa

7.

2) Utafanyika Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji kwa kila Kitongoji na kila Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza majina ya mipaka ya Vitongoji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika katika mahali pa matangazo ya uchaguzi siku hamsini (50) kabla ya siku ya Uchaguzi.

RASIMU

Halmashauri ya Kijiji

(1) Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji hawatapungua 15 na hawatazidi 25, ambao ni:-

. Mwenyekiti wa Kijiji;
a. Wenyeviti wa Vitongoji vilivyomo katika eneo la Kijiji; na
b. Wajumbe watakaochaguliwa wakiwemo wanawake ambao idadi yao haitakuwa chini ya robo ya wajumbe wote wa Halmashauri ya Kijiji.

(2) Afisa Mtendaji wa Kijiji atakuwa Katibu wa Halmashauri ya Kijiji

Maelekezo kuhusu Uchaguzi

8. (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya uchaguzi siku zisizopungua 28 kabla ya siku ya uchaguzi.

(2) Maelekezo ya uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hii yataelekeza mambo yafuatayo:

a. tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi;
b. muda na sehemu ya kuandikishia wapiga kura

c. muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;

d. kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura washiriki uchaguzi

e. kuwataka wakazi wenye umri wa miaka 21 au zaidi wanaotaka

kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji,ujumbe wa Halmashauri ya

Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji wachukue fomu za kugombea

Orodha ya wapiga

zitakazopatikana kwenye Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa

kura 9. Uchaguzi;

f. tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kuagiza kwamba muda wa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea hautazidi siku saba (7);

g. siku ambayo uteuzi utafanyika na mahali pa matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa ili wapiga kura wazione;

h. muda wa kutoa pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;

i. tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

j. kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi ambacho hakitazidi siku saba (7) kuanzia tarehe ya uteuzi; na

k. masuala mengineyo yanayohusiana na Uchaguzi.

3. Uandikishaji wa Orodha ya wapiga kura katika Kitongoji kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji,Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji utafanyika siku sitini (60) kabla ya siku ya uchaguzi na utafanywa na watumishi wa umma.Watendaji wa vijiji, Mitaa na Kata hawataruhusiwa kuandikisha na kuandaa orodha

RASIMU

ya wapiga kura

Sifa za wapiga kura

10. b. Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajiri.

Kupoteza sifa

11. 3. Vituo vya uandikishaji wa orodha ya wapiga kura vitafunguliwa kuanzia saa 1.30 asubuhi na kufungwa saa 12.00 jioni.

Sifa za mgombea

12 4. Uandikishaji wa Orodha ya wapiga utafanyika katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna majengo ya umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa.

5. Vituo vya uandikishaji wa orodha ya wapiga kura vitafunguliwa saa 1:30 asubuhi na kufungwa saa kumi(10:00) jioni

6. Vyama vya siasa vitaruhusiwa kuwepo wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

7. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika mahali pa matangazo ya uchaguzi Orodha ya wapiga kura na kutunza kumbukumbu yake.

8. Mkazi yeyote wa Kitongoji au vyama vya siasa vitakuwa na haki ya kukagua Orodha ya wapiga kura katika

RASIMU

muda wa siku nne (4) tangu tarehe orodha ya wapiga kura ilipobandikwa mahali pa matangazo ya uchaguzi ili kutoa pingamizi au maoni ya usahihi wa Orodha hiyo na anaweza kuomba:-

(a) Orodha irekebishwe kwa kuongeza jina lake au jina la mkazi; au

(b) Orodha irekebishwe kwa kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa hana sifa ya kupiga kura katika Kitongoji husika.

(8) Pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atalitolea uamuzi na kurekebisha orodha ya wapiga kura iliyotangazwa katika muda wa siku tano (5) kuanzia tarehe ya kuwasilishwa pingamizi hilo.

(9) Mtu yeyote au chama cha siasa ambacho hakitaridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kitawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ataishughulikia rufaa hiyo katika muda wa siku tano (5) baada ya kupokea rufaa hiyo.

(10) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (8) ya Kanuni hii utakuwa wa mwisho.

Mkazi yeyote wa Kitongoji atakuwa na haki ya kupiga kura ikiwa:-

. ni raia wa Tanzania;
a. ana umri wa miaka 18 au zaidi;
b. ni mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji; na
c. hana ugonjwa wa akili.

Mkazi yeyote wa Kitongoji hatakuwa na haki ya kupiga kura ikiwa:-

d. si raia wa Tanzania;
e. hajatimiza umri wa miaka 18;
f. si mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji; na
g. ana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari

RASIMU

anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

(1) Mkazi yeyote wa Kitongoji anaweza kugombea uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji ikiwa:-

h. ni raia wa Tanzania;
i. ana umri wa miaka 21 au zaidi;
j. ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
k. ana kipato halali cha kumwezesha kuishi;
l. ni mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji;
m. ni mwanachama na amedhaminiwa na chama cha siasa;

g. asiwe amepatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu na kuhukumiwa adhabu ya kifungo cha miezi 6 au zaidi au adhabu ya kifo; na
h. hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Siku ya uteuzi. 13.

(1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Uenyekiti wa Kitongoji siku zisizopungua ishirini (20) kabla ya tarehe ya Uchaguzi.

2. Siku ya uteuzi, wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya saa kumi (10.00) kamili jioni baada ya hapo fomu hazitapokelewa ili kuruhusu kufanyika kwa uteuzi wa wagombea kutokana na fomu zilizowasilishwa.
3. Uteuzi utafanyika kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi hadi saa kumi na dakika kumi na tano(10.15) jioni ya siku ya uteuzi.
4. Baada ya uteuzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika mahali pa matangazo ya uchaguzi majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya Uenyekiti, Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Uenyekiti wa Kitongoji.
5. Ikiwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, utaratibu wote wa uteuzi utaanza upya.

Kutengua uteuzi 14.

RASIMU

6. Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kijiji kutokana na kifo au sababu nyingine yeyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kufanya uteuzi mpya siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu siku ya uteuzi uliotenguliwa.

(2) Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kitongoji kutokana na kifo au sababu nyingine yeyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kufanya uteuzi mpya siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu siku ya uteuzi uliotenguliwa

2. Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na wagombea wa Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kutokana na kifo au sababu nyingine yoyote Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(4) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kijiji kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(5) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Kitongoji kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(6) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

Pingamizi dhidi ya uteuzi.

15. (1) Mgombea ambaye hakuteuliwa na ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumtaka Msimamizi

RASMI

Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamteua au atatengua uteuzi uliofanyika kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni hizi.

2. Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii itawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili (2) tangu uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili (2) kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

3. Mgombea au mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 16 katika muda usiozidi siku nne (4) kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi

4. Kamati ya Rufaa itasikiliza na kutoa uamuzi kuhusu uteuzi wa mgombea katika muda usiozidi siku nne (4) tangu siku ya kupokea rufaa.

5. Uamuzi wa Kamati ya Rufaa kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la uteuzi utakuwa wa mwisho.

6. Mgombea au mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua kesi Mahakama ya Wilaya baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

Kamati ya Rufaa 16. 7. Kutakuwepo na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya itakayoteuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa ambayo itasikiliza malalamiko ya uteuzi wa mgombea wa uchaguzi katika kila Wilaya.

2. Kamati ya Rufaa itateuliwa siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.

3. Kamati ya Rufaa itakayoteuliwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa na wajumbe

wafuatao:-

a. Katibu Tawala wa Wilaya au Afisa mwingine wa umma atakayeteuliwa ambaye atakuwa Mwenyekiti;

b. Viongozi wawili (2) wa dini kutoka madhehebu tofauti yaliyopo katika eneo la wilaya;

Utashi wa wajumbe wa Kamati ya rufaa

17

c. Afisa yeyote kutoka Taasisi ya Umma iliyoko katika wilaya husika; na

d. Afisa yeyote wa umma anayefanya kazi katika ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa katibu ambaye hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kampeni za uchaguzi

4. Bila kuathiri kanuni ndogo ya 3 ya kanuni hizi, endapo mojawapo ya nafasi ya wajumbe waliotajwa kwenye kanuni ndogo ya 3 ya kanuni hizi haipo katika eneo la wilaya basi uteuzi wa mjumbe utazingatia hali halisi ya eneo husika.

18

Mtu yeyote hatateuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Rufaa iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 16 endapo:-

(i) anahusika na uteuzi wa wagombea;

(ii) ni Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iii ni kiongozi wa ngazi yeyote wa chama cha siasa; na

(iv) ni mtumishi wa Halmashauri.

(1 ) Kampeni za uchaguzi zitaanza siku moja (1) baada ya uteuzi wa wagombea na zitamalizika siku moja (1) kabla ya siku ya uchaguzi.

(2) Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa kufuata ratiba itakayowasilishwa na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa na kuratibiwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha ratiba ya kampeni za uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye atahakikisha kunakuwepo ulinzi na usalama katika mikutano

RASIMU

ya kampeni.

(4) Ratiba ya kampeni za uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi itakuwa taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi.

(5) Kampeni za uchaguzi zitaanza saa mbili (2.00) asubuhi mpaka saa kumi na moja (11.00) jioni ya kila siku ya kampeni.

Masharti ya kampeni

19 Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa kutumia rushwa, takrima, kashfa, lugha za matusi, ubaguzi wa kijinsia, kidini, ukabila au wa namna yoyote ile ambao matokeo yake ni kumbagua mtu.

Utaratibu wa kupiga kura

20 0. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa viti maalum wanawake, utafanyika katika vitongoji vilivyomo katika Kijiji.

2. Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna ya kumwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa.

3. Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililowazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

4. Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajampatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, atajiridhisha kama jina la mpiga kura limeorodheshwa katika orodha ya wapiga kura

5. Bila kuathiri Kanuni Ndogo ya (4) hapo juu, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza pia kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye orodha ya wapiga

RASIMU

kura.

6. Aina ya vitambulisho ambavyo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe ni pamoja na vifuatavyo:

a. kitambulisho cha mpiga kura;
b. kitambulisho cha kazi;
c. hati ya kusafiria;
d. kadi ya benki;
e. kadi ya bima ya afya; au
f. kitambulisho cha shule au chuo.
g. Leseni ya udereva

7. Ikiwa mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote, lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

8. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atampatia mpiga kura karatasi nne (4) za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo:-

a. Mwenyekiti wa Kijiji;

b. Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;
c. Wajumbe wa viti maalum wanawake; na
d. Mwenyekiti wa Kitongoji.

9. Kura zitapigwa kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi mpaka saa nane (8.00) mchana.

10. Kura zitakuwa za siri na zitapigwa katika majengo ya

RASIMU

umma au sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataiteua baada ya kushauriana na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa.

11. Siku ya kupiga kura, endapo atatokea mpiga kura ambaye ana ulemavu wa macho, ulemavu wowote wa kimaumbile au hajui kusoma na kuandika, anaweza kumuomba mtu aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Mgombea au Mwakilishi wake.

Karatasi za kura 20

12. Kutakuwa na kawaida za kupigia kura ambazo zitakuwa na nembo ya Halmashauri husika kama zinavyooneshwa kwenye fomu chini ya Kanuni hizi.

2. Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ndogo ya (1) ya Kanuni hii, karatasi maalum za kupigia kura zitakuwa na sifa zifuatazo:

a. Sehemu mpiga kura atakapoandika jina la mgombea anayempigia kura;

b. Sehemu ambapo mpiga kura ataandika jina la chama cha siasa cha mgombea aliyempigia kura; na
c. uwezo wa kukunjwa kwa urahisi.

Kuhesabu kura 21

9. Wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kuwepo katika kituo cha kuhesabia kura:-

i. Msimamizi wa Uchaguzi;

b. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
c. Mgombea;
d. Mwakilishi wa Mgombea;
e. Polisi, Mgambo au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na
f. Mwangalizi wa Uchaguzi.

2. Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajaanza

RASIMU

kuhesabu kura atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au wawakilishi wao:-

b. kuhakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

b. atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;
c. atakagua lakiri na kuona kama imefunguliwa au haijafunguliwa;
d. atakata lakiri; na
e. atafungua sanduku la kupigia kura.

3. Kura zitahesabiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwenye Kitongoji ambako uchaguzi umefanyika mbele ya Wagombea au Wawakilishi wao.

Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji

22 4. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

2. Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi ambaye atatangazwa kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

3. Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji yatajazwa kwenye fomu maalum ambayo itasainiwa na Wagombea au Wawakilishi wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo.

Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

23. (1) 1) Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa Viti Maalum Wanawake yatajazwa kwenye fomu maalum ambayo itasainiwa na Wagombea au Wawakilishi wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo na nakala kuwasilishwa Ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa ajili ya kujumlishwa na kutangaza mshindi au washindi wa kila nafasi iliyogombewa.

RASIMU

(2) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume utakuwa kama ifuatavyo:

. endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;

b. endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

c. endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji; na

d. endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza mshindi na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao, ambao watatangazwa kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

(3) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi la wagombea wa viti maalum wanawake utakuwa kama ifuatavyo:

. endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na

utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;

b. endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza

RASIMU

kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

c. endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi wa Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji; na

d. endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wote au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao ambao watatangazwa kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Mwenyekiti

24 2. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Kijiji na kujaza jumla ya kura katika fomu maalum.

2. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji.

3. Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi ambaye atatangazwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji.

Matendo yasiyobatilisha matokeo ya uchaguzi

25 Kwa mujibu wa Kanuni hizi, kutokuwepo kwa wagombea au wawakilishi wao wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo au kukataa kusaini fomu ya matokeo hakutazuia wala kubatilisha utekelezaji wa shughuli yoyote ya uchaguzi.

Kuahirisha Upigaji Kura

26. Siku ya kupiga kura endapo litatokea tukio litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ili mradi zisizidi siku saba (7) tangu siku ya uchaguzi ulipoahirishwa.

Malalamiko

27. (1) Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uendeshaji wa uchaguzi

RASIMU

Kuhusu Uendeshaji wa uchaguzi

atakuwa na haki ya kupeleka malalamiko yake Mahakama ya Wilaya katika muda wa siku thelathini (30) baada ya siku ya kutangaza matokeo ya uchaguzi.

(2) Malalamiko ya uchaguzi yatakayowasilishwa Mahakama ya Wilaya ni yale tu yatakayokuwa yanahusu ukiukwaji wa utaratibu wa uchaguzi uliowekwa na Kanuni hizi.

Nafasi wazi

28. (1) Nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:-

b. kifo cha Mwenyekiti au Mjumbe;
c. mwenyekiti au Mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;
d. mwenyekiti au mjumbe kuondokewa na sifa za kuwa mgombea;
e. kubatilishwa kwa matokeo ya uchaguzi;
f. kukoma kuwa mwanachama wa chama cha siasa kilicho mdhamini;
g. kuhama Kijiji au Kitongoji;
h. endapo Mwenyekiti hataitisha mikutano mitatu (3) ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi; na
i. endapo mwenyekiti au mjumbe hatahudhuria mikutano mitatu (3) ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu ya msingi.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii, Afisa Mtendaji wa Kijiji atatoa taarifa kwa Mkurugenzi katika kipindi kisichozidi siku saba (7) tangu kutokea kwa jambo hilo.

Uchaguzi mdogo

29. (1) Mkurugenzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji siku saba (7) baada ya kupokea taarifa toka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji juu ya kuwepo kwa nafasi iliyoachwa wazi.

2. Nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa kwa kufanya uchaguzi mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.

3. Nafasi ya uenyekiti wa Kjiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji

RASIMU

itajazwa katika muda wa siku sitini (60) baada ya kutangazwa kuwa wazi.

4. Hakuna nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itakayojazwa endapo muda uliobaki ni miezi sita (6) au pungufu yake kufikia siku ya kufanyika kwa uchaguzi wa kawaida.

**Kiapo**

30. Wafuatao watatakiwa kula kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Wakili, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-

a. Msimamizi wa Uchaguzi;
b. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
c. Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Rufaa; na
d. Afisa mwingine yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi.

**Masharti ya Kuwalinda Wasimamizi wa uchaguzi na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa**

31. (1) Hatua yoyote ya nidhamu au kiutawala itakayochukuliwa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au Afisa yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa uchaguzi ambayo itathibitika kwamba ni hatua za kulipa kisasi au kumkomoa mhusika itakuwa ni batili na yeyote atakayehusika kuchukua hatua hizo atakuwa ametenda kosa la jinai chini ya Kanuni hizi.

(2) Mtu au Taasisi yoyote itakayokiuka Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii ikipatikana na hatia itahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote yaani faini na kifungo.

**Watazamaji wa ndani na nje wa Uchaguzi**

32 5. Watazamaji wa ndani na wa nje watakaopenda kutazama Uchaguzi wataruhusiwa kufanya hivyo baada ya kupata kibali cha Msimamizi wa Uchaguzi.
6. Watazamaji wa uchaguzi wa ndani na nje watafanya shughuli zao za utazamaji kwa gharama zao wenyewe.

**Makosa ya Uchaguzi**

33 (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda makosa ya Uchaguzi ikiwa:-

g. ataharibu orodha ya wapiga kura;
h. atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au

RASIMU

kugombea uenyekiti au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Mwenyekiti wa Kitongoji;

i. ataharibu karatasi za wagombea;

j. ataghushi karatasi za uteuzi;

k. atapiga kura zaidi ya moja kwa ajili ya kumchagua mgombea mmoja;

l. atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga uchaguzi;

m. atafanya kampeni siku ya uchaguzi;

n. ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au chama cha siasa katika mita mia tatu (300) kutoka kwenye Kituo cha Uchaguzi;

o. atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi kutekeleza majukumu yake;

p. atakiuka masharti ya kiapo chake;

q. atafanya jambo lolote kinyume na Kanuni za Uchaguzi;

r. atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa mgombea mmoja; na

s. atavunja masharti ya kampeni za uchaguzi.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali namba 315 na 316 ya Mwaka 2004

34 Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji Katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2004 zinafutwa.

**FOMU NA. 1**

## FOMU YA UCHAGUZI

## FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI/KIJIJI

***( Chini ya kanuni ya 7)***

Kitongoji……………………..

Kijiji…………………………

Kata………………………….

Halmashauri ya Wilaya……..

### SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA

(Ijazwe na anayeomba kugombea)

1. Jina…………………………………………..
2. Jinsi (Me/Ke)..………………………………
3. Uraia ………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa……...…………………...
5. Mahali unapoishi katika Kitongoji/Kijiji………………
6. Kazi/shughuli yako halali……………………
7. Uwezo wako wa Kusoma na Kuandika

a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
c. Kusoma Kiingereza Ndiyo/Hapana*
d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

8. Jina la chama cha siasa…………………
9. Namba ya kadi yako ya uanachama………… tarehe ilipotolewa…………mahali ilipotolewa…………

RASIMU

10. Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo

11. Saini ……tarehe ………

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

*(Chini ya kanuni ya 8(2) (d) )*

(*Ijazwe na Ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa …………………..ni mwanachama na amedhaminiwa na ……………………………………………………..

   (*Taja jina la chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na chama cha siasa ………………………………
3. Saini………………………….. Tarehe ………………………………….
4. Wadhifa…………………………………………………… ……………..
5. Anwani:…………………………………………………… ………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa……………………………………..

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu…………………………………………………….

RASIMU

2. Muda (saa)……………………………………………………………………...
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………………………..
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………. ………………….
5. Tarehe…………………………………………………………………………..

6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………………………

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa……………………………………………
2. Sababu………………………………………………………………………

………………………………………………………………………….

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………………………….
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………………….
5. Tarehe……………………………………………………………………
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au

mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji………………………………………….

RASIMU

**FOMU NA. II**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI/VITI MAALUM**

(*Chini ya kanuni ya 7* )

Kijiji………………………………………..................................

Kata…………………………………………………………….

Halmashauri ya Wilaya ya………………………………….

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**

**(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)**

1. Jina: ……………………………………………………………………..
2. Jinsi (Me/Ke)………………………………………………………………
3. Uraia …………………………………………………………………….
4. Tarehe ya kuzaliwa ……..…………………………………………………
5. Kitongoji………………………………………………………………………..
6. Kazi/shughuli yako halali…………………………………………………….
7. Uwezo wako wa kusoma na kuandika:

a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*

b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
c. Kusoma Kiingereza ndiyo/Hapana*
d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

RASIMU

8. Jina la Chama chako cha Siasa……………………
9. Namba ya kadi yako ya uanachama……………… tarehe iliyotolewa……………..mahali ilipotolewa………
10. Nathibitisha kwamba habari zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo

Saini …….tarehe …………………………..

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa……………..ni mwanachama na

   amedhaminiwa na ……………………………………

   (*Taja jina la chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na chama cha siasa ………
3. Saini:…………………………Tarehe……………
4. Wadhifa……………………………………………
5. Anwani……………………………………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa………………

RASIMU

**SEHEMU D: KURUDISHA FOMU**

**(***Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi***)**

1. Tarehe ya kupokea fomu…………………………
2. Muda (saa) …………………………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………….
5. Tarehe…………………..
6. Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………….

**SEHEMU E: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa…………………

2

.Sababu………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi……………

4.Saini ya Msimamizi wa Uchaguzi ……………………

5.Tarehe……………………………………………….

Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………..

RASIMU

**FOMU NA. III**

## FOMU YA UCHAGUZI

## FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI

*( Chini ya kanuni ya 6)*

Kitongoji…………………………

Kijiji………………………………

Kata………………………………

Halmashauri ya …………………

### SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA

(Ijazwe na anayeomba kugombea)

1. Jina………………………………………………
2. Jinsi(Me/Ke)...…………………………………
3. Uraia ……………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa…….………………………
5. Mahali unapoishi katika Kijiji……………………
6. Kazi/shughuli yako halali…………………………

7. Uwezo wako wa Kusoma na Kuandika

   a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
   b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
   c. Kusoma Kiingereza Ndiyo/Hapana*
   d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

8. Jina la Chama chako cha Siasa……………………

9.Namba ya Kadi yako ya Uanachama…………….

7. Tarehe ilipotolewa……………mahali ilipotolewa……………

RASIMU

Nathibitisha kwamba habari zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo

Saini ……………………..tarehe ……………………

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa ………………………….ni mwanachama na amedhaminiwa na ……………………………………………

(*Taja jina la Chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na Chama cha Siasa ……………
3. Saini………………………….. Tarehe ………………
4. Wadhifa…………………………………………………
5. Anwani:…………………………………………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa……………………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu……………………………
2. Muda (saa)…………………………………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………
4. Saini ya Msimamizi wa Msaidizi Uchaguzi……………..
5. Tarehe…………………………………
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi au

Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………………

**SEHEMU D: UTEUZI**

RASIMU

(*Ijazwe na Msimamizi wa Uchaguzi siku ya Uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa………………………
2. Sababu…………………………………………………….

    ………………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………...
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………..
5. Tarehe…………………………………..
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au

Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kijiji……………….

RASIMU

**FOMU NA.IV**

## ORODHA YA WAPIGA KURA

*( Chini ya kanuni ya 8 )*

Kitongoji……………………………………………………

Kijiji…………………………………………………………..

Kata…………………………………………………………

Halmashauri ya Wilaya ya…………………………………

| Na. | Jina la Mpiga Kura | Jinsi | Umri | Nyumba/Kiwanja Na……… | Saini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

RASIMU

**FOMU NA. V**

**KARATASI ZA KUPIGIA KURA ZA MWENYEKITI WA KIJIJI**

***(Chini ya Kanuni Na. 20)***

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA**

**MWENYEKITI WA KIJIJI OKTOBA, 2009**

Nembo ya Halmashauri

**UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI**

**ANDIKA JINA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA**

| 1 | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA |
| --- | --- | --- |
| | | |

RASIMU

**FOMU NA. VI**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI,**

***(Chini ya Kanuni ya 20)***

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA**

**MWENYEKITI WA KITONGOJI OKTOBA, 2009**

Nembo ya Halmashauri

**UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI**

**ANDIKA JINA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MWENYEKITI WA KITONGOJI**

| 1 | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA |
|---|---|---|
| | | |

RASIMU

**FOMU NAMBA VII**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MJUMBE WA HALMASHAURI**

Nembo ya Halmashauri

**ANDIKA JINA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI.**

| | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |

RASIMU

**FOMU NA VIII**

KARATASI YA KUPIGIA KURA ZA WAGOMBEA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI VITI MAALUM

***(Chini ya Kanuni ya 20)***

KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA

WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI VITI MAALUM OKTOBA, 2009

Nembo ya Halmashauri

**ANDIKA JINA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MJUMBE VITI MAALUM KATIKA HALMASHAURI YA KIJIJI.**

| | **JINA LA MGOMBEA** | **JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA** |
|---|---|---|
| **1** | | |
| **2** | | |
| **3** | | |
| **4** | | |
| **5** | | |
| **6** | | |
| **7** | | |
| **8** | | |

RASIMU

**FOMU NA. IX**

FOMU YA MATOKEO YA MWENYEKITI WA KIJIJI/KITONGOJI

***(Chini ya Kanuni 22 na 23(1))***

| Na. | Jina la Mgombea | Chama cha Siasa/Binafsi | Kura alizopata | Saini ya Mgombea au Mwakilishi wake |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |

RASIMU

Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura………………………………………………..

Idadi ya waliopiga kura……………………………………………………………

Idadi ya kura zilizoharibika…………………………………………………………..

Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………………………....

Saini…………………………………………………………tarehe……… …………

Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi/Afisa Mtendaji wa Kijiji…………………………………………………………………… …………..

**FOMU NA. X**

FOMU YA MATOKEO YA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI/VITI MAALUM

***(Chini ya kanuni ya 23)***

| Na. | Jina la Mgombea | Chama cha Siasa | Kura alizopata | Saini ya Mgombea au Mwakilishi wake |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |

Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura……………………………………………..

Idadi ya waliopiga kura…………………………………………………………

Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa……………………………………………..

Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………………………………....

Saini……………………tarehe…………………

Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi/Afisa Mtendaji wa Kijiji……………………………………………………………………………………..

RASIMU

**MIZENGO K. P . PINDA (MB)**

**WAZIRI MKUU**

**DAR ES SALAAM**

Tarehe……………….2009

**TANGAZO LA SERIKALI NA. …. la tarehe …………**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),**

---

**SURA 288**

---

**KANUNI**

---

**Zimetungwa chini ya Kifungu ……**

---

## KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA MTAA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MTAA KATIKA MAMLAKA ZA MIJI ZA MWAKA, 2009

Jina

1. Kanuni hizi ziitwe Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka, 2009.

Tarehe ya kuanza kutumika

2 Kanuni hizi zitatumika katika Mitaa yote ilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Miji na zitaanza kutumika tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3 Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyotamkwa vinginevyo:-

"Afisa Mtendaji wa Kata" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kata na ni pamoja na Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata kwa mujibu wa Kanuni hizi;

'Afisa Mtendaji wa Mtaa' maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Mtaa na ni pamoja na Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Mtaa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

Sura 258

"Chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

'Mtaa' maana yake ni sehemu ya Kata iliyopo kwenye eneo la Mamlaka ya

RASIMU

Sura 288

Mji kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"Mahali pa matangazo ya uchaguzi" maana yake ni sehemu iliyotengwa maalum au iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo, taarifa za Mtaa na taarifa mbalimbali za uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Mtaa na ambaye ama ana Kaya au anaishi katika Kaya au Taasisi iliyopo katika eneo la Mtaa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji na ni pamoja na afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi" maana yake ni Afisa Mtendaji wa Mtaa na ni pamoja na Afisa yeyote wa Umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi wakati wa uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji ambamo kuna Mitaa inayofanya uchaguzi na ni pamoja na Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

Sura 357

"Raia" maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

"Orodha ya wapiga kura" maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

" Siku ya uteuzi" maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea;

"Uchaguzi" maana yake ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa;

"Wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao Uchaguzi wa kawaida au Uchaguzi mdogo unatakiwa ufanyike kwa mujibu wa Kanuni hizi na unaanzia tarehe ambayo Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya uchaguzi na kumalizika mara baada ya kutangaza majina ya wagombea waliochaguliwa."

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

RASMU

| | | |
|---|---|---|
| Kuzingatia Sheria, Kanuni, matangazo na maelekezo | 4. | Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa na Afisa mwingine wa Umma atakayehusika na uendeshaji wa uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia uchaguzi huo kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Maelekezo na Matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi. |
| Tangazo la Uchaguzi kwa Umma | 5. | (1)Waziri atatoa Tangazo la Uchaguzi kwa Umma katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa Nchi nzima siku tisini (90) kabla ya siku ya Uchaguzi ili Umma uweze kujiandaa kwa ajili ya Uchaguzi.<br><br>(2) Tangazo litakalotolewa na Waziri kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii litaelekeza mambo yafuatayo:-<br><br>a. ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika; na<br><br>b. masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi. |
| Majina na mipaka ya Mitaa | 6. | (1)Utafanyika Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika kila Mtaa na kila Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza majina na mipaka ya Mitaa iliyopo katika eneo la Halmashauri husika katika mahali pa matangazo ya Uchaguzi siku hamsini (50) kabla ya siku ya Uchaguzi<br><br>1. Wajumbe wa Kamati ya Mtaa watakuwa:- |
| Wajumbe wa Kamati ya ya Mtaa | 7 | a. Mwenyekiti wa Mtaa;<br><br>(1) Wajumbe wasiozidi sita (6) na wasiopungua wanne (4) watakaochaguliwa na wakazi wa Mtaa, wawili kati yao wakiwa wanawake.<br><br>(2) Afisa Mtendaji wa Mtaa atakuwa Katibu wa Kamati ya Mtaa. |
| Maelekezo kuhusu Uchaguzi | 8 | (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya Uchaguzi siku zisizopungua 28 kabla ya siku ya uchaguzi.<br><br>(2) Maelekezo ya uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hii yataelekeza mambo yafuatayo:<br><br>a. tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi; |

RASMU

b. muda na sehemu ya kuandikishia wapiga kura
c. muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;
d. kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura

   washiriki uchaguzi;

e. kuwataka wakazi wenye umri wa miaka 21 au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa na ujumbe wa Kamati ya Mtaa wajaze fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

f. tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea Uenyekiti wa Mtaa na Ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kuagiza kwamba muda wa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea hautazidi siku saba (7);
g. siku ambayo uteuzi utafanyika na mahali pa matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa ili wapiga kura wazione;
h. muda wa kutoa pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;
i. tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
j. kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi ambacho hakitazidi siku saba (7) kuanzia tarehe ya uteuzi; na
k. masuala mengineyo yanayohusiana na Uchaguzi.

Orodha ya wapiga Kura

9. 1. Uandikishaji wa Orodha ya wapiga kura katika Mtaa kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa utafanyika siku sitini (60) kabla ya siku ya uchaguzi na utafanywa na watumishi wa umma.Watendaji wa vijiji, Mitaa na Kata hawataruhusiwa kuandikisha na kuandaa orodha ya wapiga kura

2. Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajiri.

RASIMU

3. Vituo vya uandikishaji wa orodha ya wapiga kura vitafunguliwa kuanzia saa 1.30 asubuhi na kufungwa saa 12.00 jioni.

4. Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa vyama vya Siasa.

5. Vituo vya uandikishaji wa orodha ya Wapiga Kura vitafunguliwa kuanzia saa 1.30 asubuhi na kufungwa saa kumi(10:00) jioni

6. Vyama vya siasa vitaruhusiwa kuwepo wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

7. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika mahali pa matangazo ya uchaguzi orodha ya wapiga kura na kutunza kumbukumbu yake.

8. Mkazi yeyote wa Mtaa au vyama vya siasa vitakuwa na haki ya kukagua orodha ya wapiga kura katika muda wa siku nne (4) tangu tarehe orodha ya wapiga kura ilipobandikwa mahali pa matangazo ya uchaguzi ili kutoa pingamizi au maoni ya usahihi wa Orodha hiyo na anaweza kuomba:-

   (a) Orodha irekebishwe kwa kuongeza jina lake au jina la mkazi; na

   (b) Orodha irekebishwe kwa kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa hana sifa ya kupiga kura katika Mtaa husika.

(8) Pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atalitolea uamuzi na kurekebisha orodha ya wapiga kura

RASIMU

iliyotangazwa katika muda wa siku tano (5) kuanzia tarehe ya kuwasilishwa pingamizi hilo.

(9) Mtu yeyote au chama cha siasa chenye usajili wa kudumu ambacho hakitaridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kitawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ataishughulikia rufaa hiyo katika muda wa siku tano (5) baada ya kupokea rufaa hiyo.

(10) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (6) ya Kanuni hii utakuwa wa mwisho.

**Sifa za Wapiga Kura**

10. Mkazi yeyote wa Mtaa atakuwa na haki ya kupiga kura ikiwa:-

a. ni raia wa Tanzania;
b. ana umri wa miaka 18 au zaidi;
c. ni mkazi wa kawaida wa eneo la Mtaa; na
d. hana ugonjwa wa akili.

**Kupoteza Sifa**

11. Mkazi yeyote wa Mtaa hatakuwa na haki ya kupiga kura ikiwa:-

a. si raia wa Tanzania;
b. hajatimiza umri wa miaka 18;
c. si mkazi wa kawaida wa eneo la Mtaa; na
d. ana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

**Sifa za Mgombea**

12 (1) Mkazi yeyote wa Mtaa anaweza kugombea Uenyekiti wa Mtaa au Ujumbe wa Kamati ya Mtaa ikiwa:-

a. ni raia wa Tanzania;
b. ana umri wa miaka 21 au zaidi;
c. ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
d. ana kipato halali cha kumwezesha kuishi;
e. ni mkazi wa kawaida wa eneo la Mtaa;
f. ni mwanachama na amedhaminiwa na chama cha siasa;
g. asiwe amepatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu na kuhukumiwa adhabu ya kifungo cha miezi 6 au zaidi au adhabu ya kifo; na
h. hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

RASIMU

**Siku ya Uteuzi**

13. (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Uenyekiti na Ujumbe wa Kamati ya Mtaa siku zisizopungua ishirini (20) kabla ya tarehe ya Uchaguzi.

2. Siku ya uteuzi, wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya saa kumi (10.00) kamili jioni baada ya hapo fomu hazitapokelewa ili kuruhusu kufanyika kwa uteuzi wa wagombea kutokana na fomu zilizowasilishwa.
3. Saa ya uteuzi itakuwa kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi hadi saa kumi na dakika kumi na tano (10.15) jioni ya siku ya uteuzi.
4. Baada ya uteuzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika mahali pa matangazo ya uchaguzi majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa na ujumbe wa Kamati ya Mtaa.
5. Ikiwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, utaratibu wote wa uteuzi utaanza upya.

**Kutengua Uteuzi**

14. (1) Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa Uenyekiti wa Mtaa kutokana na kifo au sababu nyingine yeyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kufanya uteuzi mpya siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu siku ya uteuzi uliotenguliwa.

(2) Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na wagombea wa Ujumbe wa Kamati ya Mtaa kutokana na kifo au sababu nyingine yoyote Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(3) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa uenyekiti wa Mtaa kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

(4) Endapo baada ya uteuzi hakutakuwa na mgombea wa Ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa sababu ya kifo au kwa sababu nyingine yoyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi siyo zaidi ya siku kumi (10) tangu tarehe ya kutengua uteuzi uliofanyika.

**Pingamizi dhidi ya Uteuzi**

15. (1) Mgombea ambaye hakuteuliwa na ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kujaza fomu ya pingamizi na kumtaka Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi

RASMU

Msaidizi wa Uchaguzi atamteua au atatengua uteuzi uliofanyika kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni hizi.

2. Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii itawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili (2) tangu uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili (2) kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.
3. Mgombea au Mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 15 katika muda usiozidi siku nne (4) kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.
4. Kamati ya Rufaa itasikiliza na kutoa uamuzi kuhusu uteuzi wa mgombea katika muda usiozidi siku nne (4) tangu siku ya kupokea rufaa.
5. Uamuzi wa Kamati ya Rufaa kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la uteuzi utakuwa wa mwisho.
6. Mgombea au Mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua kesi Mahakama ya Wilaya baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

Kamati ya Rufaa

16 1. Kutakuwepo na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya itakayoteuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa kwa kuzingatia hali halisi ya Wilaya husika ambayo itasikiliza malalamiko ya uteuzi wa mgombea wa uchaguzi katika kila Wilaya.

2. Kamati ya Rufaa itateuliwa siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.
3. Kamati ya Rufaa itakayoteuliwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii itakuwa na wajumbe wafuatao:-

   a. Katibu Tawala wa Wilaya au Afisa mwingine wa umma atakayeteuliwa ambaye atakuwa Mwenyekiti;
   b. Viongozi wawili (2) wa dini kutoka madhehebu tofauti yaliyopo katika eneo la wilaya;
   c. Afisa yeyote kutoka Taasisi ya Umma iliyoko katika wilaya husika; na
   d. Afisa yeyote wa umma anayefanya kazi katika ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa katibu ambaye

RASIMU

hatakuwa na haki ya kupiga kura.

4. Bila kuathiri kanuni ndogo ya 3 ya kanuni hizi, endapo mojawapo ya nafasi ya wajumbe waliotajwa kwenye kanuni ndogo ya 3 ya kanuni hizi haipo katika eneo la wilaya basi uteuzi wa mjumbe utazingatia hali halisi ya eneo husika.

Utashi wa Wajumbe wa Kamati ya Rufaa

17. Mtu yeyote hatateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Rufaa iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 15 endapo:-

(i) anahusika na uteuzi wa wagombea;

(ii) ni Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iii ni kiongozi wa ngazi yeyote wa chama cha siasa; na

(iv) ni mtumishi wa Halmashauri.

Kampeni za uchaguzi

18. (1 ) Kampeni za uchaguzi zitaanza siku moja (1) baada ya uteuzi wa wagombea na zitamalizika siku moja (1) kabla ya siku ya uchaguzi.

(2) Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa kufuata ratiba itakayowasilishwa na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa na kuratibiwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha ratiba ya kampeni za uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye atahakikisha kunakuwepo ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni.

(4) Ratiba ya kampeni za uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi itakuwa taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi.

(5) Kampeni za uchaguzi zitaanza saa mbili (2.00) asubuhi mpaka saa kumi na moja (11.00) jioni ya kila siku ya kampeni.

Masharti ya kampeni

19 Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa kutumia rushwa, takrima, kashfa, lugha za matusi, ubaguzi wa kijinsia, kidini, ukabila au wa namna yoyote ile ambao matokeo yake ni kumbagua mtu.

RASIMU

Utaratibu wa kupiga kura 20

1. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa utafanyika katika Mtaa.

2. Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna ya kumwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa.

3. Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililowazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

4. Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajampatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, atajiridhisha kama jina la mpiga kura huyo limeorodheshwa katika orodha ya wapiga kura

5. Bila kuathiri Kanuni Ndogo ya (4) hapo juu, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza pia kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye orodha ya wapiga kura.

6. Aina ya vitambulisho ambavyo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe ni pamoja na vifuatavyo:

   a. kitambulisho cha mpiga kura;
   b. kitambulisho cha kazi;
   c. hati ya kusafiria;
   d. kadi ya benki;
   e. kadi ya bima ya afya; au
   f. kitambulisho cha shule au chuo
   g. leseni ya udereva.

RASIMU

7. Ikiwa mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote, lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, utambuzi utafanywa na wakazi wa eneo husika  na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamruhusu mtu huyo kupiga kura.

8. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atampatia mpiga kura karatasi tatu (3) za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo:-

   a. Mwenyekiti wa Mtaa;

   b. Wajumbe wa Kamati ya Mtaa; na
   c. Wajumbe wa viti maalum.

9. Kura zitapigwa kuanzia saa mbili (2.00) asubuhi mpaka saa nane (8.00) mchana.

10. Kura zitakuwa za siri na zitapigwa katika majengo ya umma au sehemu yeyote ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataiteua baada ya kushauriana na wagombea au wawakilishi wao au vyama vya siasa.

11. Siku ya kupiga kura, endapo atatokea mpiga kura ambaye ana ulemavu wa macho au ulemavu wowote wa kimaumbile au hajui kusoma na kuandika, anaweza kumuomba mtu aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, mgombea au mwakilishi wake.

Karatasi za kura 21

1. Kutakuwa za kawaida za kupigia kura ambazo zitakuwa na nembo ya Halmashauri husika kama zinavyooneshwa kwenye fomu chini ya Kanuni hizi.

RASIMU

2. Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii, karatasi za kupigia kura zitakuwa na sifa zifuatazo:-

a. Sehemu mpiga kura atakapoandika jina la mgombea anayempigia kura;

b. Sehemu ambapo mpiga kura ataandika jina la chama cha siasa cha mgombea aliyempigia kura; na
c. uwezo wa kukunjwa kwa urahisi.

Kuhesabu kura 22 1. Wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kuwepo katika kituo cha kuhesabia kura:-

a. Msimamizi wa Uchaguzi;
b. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
c. Mgombea;
d. Mwakilishi wa Mgombea;
e. Polisi, Mgambo au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na
f. Mwangalizi wa Uchaguzi.

2. Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajaanza kuhesabu kura atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au wawakilishi wao:-

a. kuhakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

b. atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;
c. atakagua lakiri na kuona kama imefunguliwa au haijafunguliwa;
d. atakata lakiri; na
e. atafungua sanduku la kupigia kura.

3. Kura zitahesabiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwenye Mtaa ambako Uchaguzi umefanyika mbele ya Wagombea au Wawakilishi wao.

RASIMU

**Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Kamati ya Mtaa**

23. 1. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atajumlisha idadi ya kura kwa wagombea wa nafasi za Wajumbe wa Kamati ya Mtaa na kujaza jumla ya kura za kila mgombea katika fomu maalum ambayo itasainiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi pamoja na wagombea au wawakilishi wao.

2. Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Kamati ya Mtaa wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume utakuwa kama ifuatavyo:-

a. endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;

b. endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa;

c. endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa; na

d. endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza mshindi na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao, ambao watatangazwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

(3) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Kamati ya Mtaa wa kundi la wagombea wa viti maalum wanawake utakuwa kama ifuatavyo:

RASIMU

a. endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;

b. endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa;

c. endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi wa Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa; na

d. endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wote au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao ambao watatangazwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Mwenyekiti wa Mtaa

24 1. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Mtaa na kujaza jumla ya kura katika fomu maalum ambayo itasainiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi pamoja na wagombea au wawakilishi wao.

2. Matokeo ya Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa yatatangazwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kuhesabu kura kwenye Mtaa husika.

3. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Mtaa.

RASIMU

4. Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ili kumpata mshindi ambaye atatangazwa kuwa Mwenyekiti wa Mtaa

**Matendo yasiyobatilisha matokeo ya uchaguzi**

25 Kwa mujibu wa Kanuni hizi, kutokuwepo kwa wagombea au wawakilishi wao wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo au kukataa kusaini fomu ya matokeo hakutazuia wala kubatilisha utekelezaji wa shughuli yoyote ya uchaguzi.

**Kuahirisha Upigaji Kura**

26. Siku ya kupiga kura endapo litatokea tukio litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ili mradi zisizidi siku saba (7) tangu siku ya uchaguzi ulipoahirishwa.

**Malalamiko kuhusu uendeshaji wa uchaguzi**

27. (1) Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uendeshaji wa uchaguzi atakuwa na haki ya kupeleka malalamiko yake Mahakama ya Wilaya katika muda wa siku thelathini (30) baada ya siku ya kutangaza matokeo ya uchaguzi.

(2) Malalamiko ya uchaguzi yatakayowasilishwa Mahakama ya Wilaya ni yale tu yatakayokuwa yanahusu ukiukwaji wa utaratibu wa uchaguzi uliowekwa na Kanuni hizi.

**Nafasi wazi**

28. (1) Nafasi ya uenyekiti wa Mtaa na ujumbe wa Kamati ya Mtaa itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:-

a. kifo cha mwenyekiti au mjumbe;
b. mwenyekiti au mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;
c. mwenyekiti au mjumbe kuondokewa na sifa za kuwa mgombea;
d. kubatilishwa kwa matokeo ya uchaguzi;
e. kukoma kuwa mwanachama wa chama cha siasa

kilicho mdhamini;

f. kuhama Mtaa;
g. endapo Mwenyekiti hataitisha mikutano mitatu (3) ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi;na
h. endapo mwenyekiti au mjumbe hatahudhuria mikutano mitatu (3) ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu ya msingi.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya kanuni hii, Afisa Mtendaji wa Mtaa atatoa taarifa kwa Mkurugenzi katika kipindi kisichozidi siku saba (7) tangu kutokea kwa jambo hilo.

RASIMU

**Uchaguzi mdogo**

29. (1) Mkurugenzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa siku saba (7) baada ya kupokea taarifa toka kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa juu ya kuwepo kwa nafasi iliyoachwa wazi.

2. Nafasi wazi ya uenyekiti au ujumbe wa Kamati ya Mta itajazwa kwa kufanya uchaguzi mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.
3. Nafasi ya uenyekiti au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itajazwa katika muda wa siku sitini (60) baada ya kutangazwa kuwa wazi.
4. Hakuna nafasi ya uenyekiti au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itakayojazwa endapo muda uliobaki ni miezi sita (6) au pungufu yake kufikia siku ya kufanyika kwa uchaguzi wa kawaida.

**Kiapo**

30. Wafuatao watatakiwa kula kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Wakili, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-

a. Msimamizi wa Uchaguzi;
b. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
c. Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa; na
d. Afisa mwingine yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi.

**Masharti ya kuwalinda Wasimamizi wa Uchaguzi na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa**

31. (1) Hatua yoyote ya nidhamu au kiutawala itakayochukuliwa dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au Afisa yeyote wa Umma aliyehusika na usimamizi wa uchaguzi ambayo itathibitika kwamba ni hatua za kulipa kisasi au kumkomoa mhusika itakuwa ni batili na yeyote atakayehusika kuchukua hatua hizo atakuwa ametenda kosa la jinai chini ya Kanuni hizi.

(2) Mtu au Taasisi yoyote itakayokiuka Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii ikipatikana na hatia itahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote yaani faini na kifungo.

RASIMU

**Watazamaji wa ndani na nje wa Uchaguzi**

32

1. Watazamaji wa ndani na wa nje watakaopenda kutazama Uchaguzi wataruhusiwa kufanya hivyo baada ya kupata kibali cha Msimamizi wa Uchaguzi.

2. Watazamaji wa uchaguzi wa ndani na nje watafanya shughuli zao za utazamaji kwa gharama zao wenyewe.

**Makosa ya Uchaguzi**

33 (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda makosa ya Uchaguzi ikiwa:-

a. ataharibu orodha ya wapiga kura;
b. atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea uenyekiti au ujumbe wa Kamati ya Mtaa;
c. ataharibu karatasi za wagombea;
d. ataghushi karatasi za uteuzi;
e. atapiga kura zaidi ya moja kwa ajili ya kumchagua mgombea mmoja;
f. atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga uchaguzi;
g. atafanya kampeni siku ya uchaguzi;
h. ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au chama cha siasa katika mita mia tatu (300) kutoka kwenye Kituo cha Uchaguzi;
i. atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi kutekeleza majukumu yake;
j. atakiuka masharti ya kiapo chake;
k. atafanya jambo lolote kinyume na Kanuni za Uchaguzi;
l. atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa mgombea mmoja; na
m. atavunja masharti ya kampeni za uchaguzi.

3. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

RASIMU

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Namba 314 ya Mwaka 2004

34. Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka ya Miji za Mwaka 2004 zinafutwa.

RASIMU

**FOMU NA. I**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UENYEKITI WA MTAA**

***(Chini ya Kanuni ya 8(2) d)***

Mtaa…………………………

Kata………………………….

Mji/Manispaa/Jiji……………

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**

(Ijazwe na anayeomba kugombea)

1. Jina………………………………………..
2. Jinsi (Me/Ke)...………………………………
3. Uraia ………………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa……...…………………...
5. Mahali unapoishi katika Mtaa………………
6. Kazi/shughuli yako halali……………………
7. Uwezo wako wa kusoma na kuandika

   a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
   b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
   c. Kusoma Kiingereza Ndiyo/Hapana*

d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

8. Jina la chama cha siasa…………………
9. Namba ya kadi ya uanachama………… tarehe ilipotolewa…………mahali ilipotolewa…………………………………………………………..…

10. Nathibitisha kwamba taarifa zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

11. Saini ………………………………………tarehe …………………..…

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe Na Msimamizi Msaidizi WA Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu………………………..
2. Muda (saa)………………………………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…… Tarehe……
5. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi au Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kata/Mtaa

**SEHEMU D: UTEUZI**

**(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)**

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa…………………….
2. Sababu………………………………………………….

…………………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………….
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …Tarehe…

RASIMU

5. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au

Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kata……………

**FOMU NA. II**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA KUGOMBEA UJUMBE WA KAMATI YA MTAA**

***(Chini ya Kanuni ya 8)***

Mtaa……………………………

Kata……………………………

Mji/Manispaa/Jiji………………

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**

(*Ijazwe na anayeomba Kugombea*)

1. Jina: ……………………………………………….

2. Jinsi (Me/Ke……………………………………….
3. Uraia ……………………………………………….
4. Tarehe ya Kuzaliwa ………………………………
5. Mahali unapoishi Mtaa…………………………….
6. Kazi/shughuli yako halali…………………………..
7. Uwezo wako wa kusoma na kuandika:

    a. Kusoma Kiswahili Ndiyo/Hapana*
    b. Kuandika Kiswahili Ndiyo/Hapana*
    c. Kusoma Kiingereza ndiyo/Hapana*
    d. Kuandika Kiingereza ndiyo/Hapana*

8. Jina la chama cha siasa……………………

9. Namba ya kadi ya uanachama……………… tarehe iliyotolewa……… mahali ilipotolewa………
10. Nathibitisha kwamba taarifa zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo



RASIMU

Saini ……………………………………..tarehe ………………

*(*futa isiyohusika)*

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

*(Chini ya Kanuni ya 11(1)(f) )*

(*Ijazwe na ofisi ya chama cha siasa*)

1. Hii ni kuthibitisha kuwa……………………………ni Mwanachama na

   amedhaminiwa na ……………………………………………………………

(*Taja jina la chama*)

2. Jina la aliyeidhinishwa na chama cha siasa ……….
3. Saini:…………………………Tarehe…………….
4. Wadhifa……………………………………………
5. Anwani……………………………………………
6. Mhuri wa ofisi ya chama cha siasa………………..

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

**(***Ijazwe Na Msimamizi Msaidizi WA Uchaguzi***)**

1. Tarehe ya kupokea fomu……………………………………….………….
2. Muda (saa) …………………………………………………………..
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………………
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………………………………
5. Tarehe……………………………………………………………………..
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi /

   Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kata/Mtaa………………………………..

**SEHEMU D: UTEUZI**

***(Chini ya Kanuni ya 12)***

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa…………………
2. Sababu……………………………………………………………

RASMU

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi……………………………………
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi
   ……………….……………………
5. Tarehe……………………………
6. Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi

   au Mhuri wa Afisa Mtendaji wa Kata/Mtaa……………………

**FOMU NA.III**

**ORODHA YA WAPIGA KURA**

*( Chini ya Kanuni ya 8 )*

Mtaa……………………………………………………………

Kata……………………………………………………………

Mji/Manispaa/Jiji…………………………………………………

| Na. | Jina la Mpiga Kura | Jinsi | Umri | Nyumba/Kiwanja Na | Saini |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

RASIMU

FOMU NA. IV

KARATASI ZA KUPIGIA KURA ZA MWENYEKITI WA MTAA

***(Chini ya Kanuni Na. 21)***

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA**

**MWENYEKITI WA MTAA OKTOBA, 2009**

Nembo ya Halmashauri

UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA MTAA

ANDIKA JINA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MWENYEKITI WA MTAA

| | **JINA LA MGOMBEA** | **JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA** |
|---|---|---|
| **1** | | |

RASIMU

FOMU NA. V

**KARATASI YA KUPIGIA KURA ZA WAGOMBEA UJUMBE WA KAMATI YA MTAA VITI MAALUM**

***(Chini ya Kanuni Na. 21)***

Nembo ya Halmashauri

**ANDIKA JINA NA CHAMA CHA MGOMBEA UNAYEMCHAGUA KUWA MJUMBE WA KAMATI YA MTAA VITI MAALUM .**

| | **JINA LA MGOMBEA** | **JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA** |
|---|---|---|
| **1** | | |
| **2** | | |

RASIMU

**FOMU NA. VI**

FOMU YA MATOKEO YA MWENYEKITI WA MTAA

***(Chini ya Kanuni 24)***

Mtaa………………………………

Kata…………………………….

Mji/Manispaa/Jiji……………………..

| Na. | Jina la Mgombea | Chama cha Siasa | Kura alizopata | Saini ya Mgombea/ Mwakilishi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |
| 11 | | | | |
| 12 | | | | |
| 13 | | | | |
| 14 | | | | |
| 15 | | | | |
| 16 | | | | |
| 17 | | | | |

Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura…………………………………………

Idadi ya waliopiga kura…………………………………………………

Idadi ya kura zilizoharibika…………………………………………………

Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………………………………

RASIMU

Saini……………………………………………………………tarehe………
……Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi/Afisa Mtendaji wa Mtaa…………………………………………

FOMU NA. V11

FOMU YA MATOKEO YA WAJUMBE WA KAMATI YA MTAA/VITI MAALUM

***(Chini ya Kanuni ya 23)***

| Na. | Jina la Mgombea | Chama cha Siasa | Kura alizopata | Saini ya Mgombea au Mwakilishi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |
| 11 | | | | |
| 12 | | | | |
| 13 | | | | |
| 14 | | | | |
| 15 | | | | |
| 16 | | | | |
| 17 | | | | |

Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura………………………………………………….

Idadi ya waliopiga kura…………………………………………………………………

Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa………………………………………………..

RASIMU

Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………………………..

Saini……………………………tarehe……………………………………………

Mhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi/Afisa Mtendaji wa Mtaa……………………………………..

RASIMU

MIZENGO K. P. PINDA (MB)

WAZIRI MKUU

DAR ES SALAAM

Tarehe …………….2009